Twende Kwa Nani?

na

Ellis P. Forsman

Twende Kwa Nani?

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Twende Kwa Nani?

Yohana 6:67-69

Yesu alipozungumza kuhusu kuwa mkate wa uzima, iliwapa shida watu wengine.

Alitumia lugha ya mfano, ambayo ilionekana kuwa ni ajabu.

Yohana 6:51-59, "*Mimi ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka mbinguni, mtu akila chakula hiki ataishi milele. Na chakula nitakachotoa mimi ni mwili wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu. Basi Wayahudi walishindana wao kwa wao wakisema, awezaje mtu huyu kutupa sisi mwili wake ili tuule? Basi Yesu akawaambia, amin,amin, nawambieni, Msipoula Mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; name nitamfufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, name hukaa ndani yake. Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi, name ni hai kwa Baba; kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi. Hiki ndicho chakula kishukacho kutoka mbinguni; si kama baba walivyokula, wakafa; bali akilaye chakula hicho ataishi milele. Maneno hayo aliyasema katika sinagogi, alipokuwa akifundisha, huko Kapernaumu.*"

Hii ilikuwa ni vigumu kuelewa; wengine walikwazwa (wale wenye imani haba).

Yohana 6:60-65, "*Basi watu wengi miongoni mwa wanafunzi wake waliposikia, walisema, Neno hili ni gumu, ni nani awezaye kulisikia? Naye Yesu akafahamu nafsini mwake ya kuwa wanafunzi wake wanalinung'unikia neno hilo, akawaambia, Je! Neno hili linawakwaza? Itakuwaje basi, mmwonapo Mwana wa Adamu akipaa huko alikokuwako kwanza? Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho tena ni uzima. Lakini kuna wengine miongoni mwenu wasioamini. Kwa maana Yesu alijua tangu mwanzo ni nani wasioamini, naye ni nani atakayemsaliti. Akasema, kwa sababu hiyo nimewaambia ya kwamba hakuna mtu awezaye kuja kwangu isipokuwa amejaliwa na Baba yangu.***"**

Wengi wa wanafunzi wake walimwacha.

Yohana. 6:66, "*Kwa ajili ya hayo wengi miongoni mwa wanafunzi wake wakarejea nyuma, wasiandamane naye tena.*"

Ikampelekea Yesu kuwauliza wale kumi na wawili:

Yohana 6:67, "*…Ninyi nanyi mwataka kuondoka?"*

Jibu la Petro linatumika kama kifungu cha somo letu…

Yahana 6:68, "*…Twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele."*

Anatambua kuwa ni Yesu pekee aliye na maneno ya uzima wa milele.

Pia anakiri imani yao katika Yeye:

Yohana 6:69, "*Nasi tumesadiki, tena tumejua ya kuwa wewe ndiwe Mtakatifu wa Mungu."*

Swali lake ni moja ambalo tunafanya vizuri kwa kuuliza leo.

Kwa maana majibu ya makusudi yetu ya kweli na kazi katika maisha, kupata maneno ya uzima wa milele, "Twende Kwa Nani?" kuna sehemu nyingi ambazo tunaweza kuzigeukia, hakika wengi wanazigeukia, lakini si sahihi. Kwa mfano, zingatia…

Twende kwa nani?

Mawazo ya wengi?

Watu wengi wanaangalia chochote ambacho wengi wanaamini.

Ambacho akili zao zinafikiria.

Chochote kilichojiri.

Lakini zingatia maneno ya Yesu, katika kuelezea mwisho wa wengi.

Math. 7:13-14, "*Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani nao waionao ni wachache.*"

Kama ukiwafuata wengi…

Wakati wa Nuhu, ungeweza kuangamia katika mafuriko.

Wakati Yoshua, ungeweza kuangamia jangwani.

Matamshi ya hekima ya wanadamu?

Wengi wanahisi kuwa hekima za kibinadamu zinaweza kuwaongoza katika kweli na uzima.

Hasa ile iliyotamkwa na maprofesa wasomi.

Lakini mawazo ya Mungu na njia zake mara zote si zetu.

Isa. 55:8-9, "*Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.*"

Hakika, Mungu amechagua kuokoa mwanadamu zaidi sana wale wanaoonekana kutegemea mawazo ya kibinadamu.

1 Wakor. 1:18-29, "*Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu. Kwa kuwa imeandikwa, Nitaharibu hekima yao wenye hekima, na akili zao wenye akili nitazikataa. Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mlete hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hakima ya dunia kuwa ni upumbavu? Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa. Kwa sababu Wayahudi wanataka ishara, na Wayunani wanatafuta hekima; bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulubiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi; bali kwao waitwao Wayahudi kwa Wayunani, ni Kristo nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu. Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu. Maana ndugu zangu angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hakima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa; bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu; tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa, naam, vitu ambavyo haviko, ili avibatilishe vile vilivyoko; mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu.*"

Je matangazo ya wahubiri?

Ni kawaida kwa watu kuwaamini wahubiri wao, kuhani, "wachungaji".

Wanafikiria hakika hawa "watu wa Mungu" hawawezi kuwa na kosa au kuwaongoza kimakosa.

Wakati, Paulo alionya jinsi ilivyorahisi kuongongozwa vibaya.

2 Wakor. 11:13-15, "*Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. Wala si ajabu. Maana shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao.*"

Na Yesu alionya kuhusu "kipofu kumuongoza kipofu".

Math. 15:12-14, "*Ndipo wanafunzi wake walipomwendea, wakamwambia wajua ya kuwa Mafarisayo waliposikia neno lile walichukizwa? Akajibu, akasema, Kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni litang'olewa. Waacheni; hao ni viongozi vipofu wa vipofu. Na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili.*"

Fikra (Imla) ya dhamira zetu?

"Acha dhamira yako iwe mwongozo wako" ni kauli mbiu ya wengi.

Lakini dhamira yetu mara nyingi haiwezi kuwa sahihi.

Paulo alimtumikia Mungu kwa dhamira njema maisha yake yote.

Matendo 23:1, "*Paulo akawakazia macho watu wa baraza, akasema, ndugu zangu, mimi kwa dhamiri safi kabisa nimeishi mbele za Mungu hata leo hivi.*"

Hata kwa wakati alipokuwa akiwatesa Wakristo!

Matendo 26:9-11, "*Kweli, mimi mwenyewe naliona ndani ya nafsi yangu kwamba yanipasa kutenda mambo mengi yaliyopingamana na jina lake Yesu Mnazareti; name nikayafanya hayo Yerusalemu; niliwafunga wengi miongoni mwa watakatifu ndani ya magereza, ni kiisha kupewa amri na wakuu wa makuhani; na walipouawa nalitoa idhini yangu. Na mara nyingi katika masinagogi yote naliwaadhibu, nikawashurutisha kukufuru, nikawaonea hasira kama mwenye wazimu, nikawaudhi hata katika miji ya ugenini.*"

Dhamira yetu ni kama saa ya ukutani, inayofanya kazi kama tu ikirekebishwa vizuri.

Mwelekeo wa hisia zetu?

Hii maranyingi utokea watu wengi wanapogeuka…

Wanaokwenda na chochote wanacho "hisi kuwa sahihi".

Wanao weka hazina katika vitu ambavyo vime "wamejisikia zaidi ya kuambiwa".

Alafu, Biblia inatangaza hatari ya kutegemea "hisia".

- Mith. 14:12, "*Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti.*"
- Mith. 28:26, "*Mwenye kujitumainia moyo ni mjinga; bali yeye aendaye kwa busara ataokolewa.*"

- Yer. 10:23, "*Ee BWANA, najua yakuwa njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake; kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu.*"

Hayupo kati ya hawa ambaye atakuwa chanzo cha kugeukia kwetu kama tunatafuta maneno ya uzima wa milele. Kama alivyokiri Petro, kuna Mmoja pekee…

Twende kwa nani?

Jesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai!

Kama Petro anavyokiri katika kifungu chetu.

Yohana 6:68-69, "*Basi Simoni Petro akamjibu, Bwana! Twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele. Nasi tume sadiki, tena tumejua, ya kuwa wewe ndiwe mtakatifu wa Mungu.*"

Yeye ndiye atupaye kila tunachohitaji:

- Yohana 6:27, "*Msikitendee kazi chakula chenye kuharibika, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele; ambacho Mwana wa Adamu atawapa kwa sababu huyo ndiye aliyetiwa muhuri na Baba, yaani Mungu.*"
- Yohana 6:35, "*Yesu akawaambia Mimi ndimi chakula cha uzima; yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe.*"
- Yohana 6:40, "*Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho.*"
- Yohana 14:6, "*Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.*"
- Yohana 6:27, "*Msikitendee kazi chakula chenye kuharibika, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele; ambacho Mwana wa Adamu atawapa, kwa sababu huyo ndiye aliyetiwa muhuri na Baba, yaani Mungu.*"

Mungu alimdhibitisha Yesu ili awe chanzo cha uzima wa milele.

- Yohana 5:36, "*Lakini ushuhuda nilio nao mimi ni mkubwa kuliko ule wa Yohana; kwa kuwa zile kazi alizonipa Baba ili nizimalize kazi hizo zenyewe ninazozitenda, zanishuhudia ya kwamba Baba amenituma.*"

- Waru. 1:4, "*Na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu.*"

Lakini, ni jinsi gani "mtu anamwendea Yesu" wakati hatembei duniani? Lazima tugeukie…

Mitume wa Kristo, waliovuviwa na Roho!

Yesu aliwaanda na kuwa himiza wanafunzi wake kuendeleza na kumaliza kazi yake.

Aliwaambia kuhusu Roho Mtakatifu.

Yohana 16:7-11, "*Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo msaidizi hatakuja kwenu, bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu. Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. Kwa habari ya dhambi kwa sababu hawaniamini mimi. Kwa habari ya haki, kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba wala hamnioni tena; kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa.*"

Ambaye angewaongoza katika kweli yote.

Yohana 16:12-13, "*Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini Yeye atakapokuja huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote, kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.*"

Kuwapokea mitume ni kumpokea Yesu.

Yohana 13:20, "*Amin,amin, nawaambieni, Yeye ampokeaye mtu yeyote nimpelekaye, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi; ampokea yeye aliyenipeleka.*"

Hivyo, mitume walikuwa ni wasemaji wa Kristo walio na mamlaka.

- 1 Wathes. 4:1-2, "*Iliyobaki, ndugu, tunakusihini na kuwaonya kwamba mwenende katika Bwana Yesu; kama mlivyopokea kwetu jinsi iwapasavyo kuenenda na kumpendeza Mungu, kama nanyi mnavyoenenda, vivyo hivyo mpate kuzidi sana. Kwa kuwa mnajua ni maagizo gani tuliyowapa kwa Bwana Yesu.*"

- 1 Wathes. 4:8, "*Basi yeye anayekataa, hakatai mwanadamu bali Mungu, anayewapa ninyi Roho wake Mtakatifu.*"

- 1 Yohana 4:6, "*Sisi twatokana na Mungu. Yeye amjuaye Mungu atusikia; yeye asiyetokana na Mungu hatusikii. Katika hili twamjua Roho wa kweli, na roho ya upotevu.*"

- Yuda 1:17, "*Bali ninyi, wapenzi, yakumbukeni maneno yaliyonenwa zamani na Mitume wa Bwana wetu Yesu Kristo."*

Walipokea vitu vyote vifaavyo katika uzima na utauwa.

2 Petr. 1:3, "*Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kunjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.*"

Hawakuona aibu kutangaza mapenzi yote ya Mungu.

- Matendo 20:20-21, "*Ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia neno lolote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba, nikiwashuhudia Wayahudi kwa Wayunani watumbie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo.*"

- Matendo 20:27, "*Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.*"

Lakini "tunakwendaje kwa mitume" wakati hawaishi duniani? Lazima tugeukie…

Neno la Mungu katika Agano Jipya!

Mitume waliandika kusudi tufaidike kutokana na uelewa wao.

Waef. 3:3-5, "*Ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo, kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache. Kwa hayo myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo. Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho.*"

Lazima tutazame maneno yao kama maagizo ya Bwana.

1 Wakor. 14:37, "*Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*"

Kwa hiyo, lazima tushikilie kile walicho fundisha.

- 2 Wathes. 2:15, "*Basi ndugu simameni imara mkayashike mapokeo mliofundishwa, ama kwa maneno ama kwa waraka wetu.*"

- 2 Wathes. 3:15, "*Lakini msimhesabu kuwa adui, bali mwonyeni kama ndugu.*"

- Yuda 1:3, "*Wapenzi nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu*

kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu."

Kama ilivyoonyeshwa na kanisa la kwanza kabisa la Yerusalemu.

Matendo 2:42, "*Wakawa wakidumu katika fundisho la Mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.*"

Maneno ya mitume yaliyotunzwa katika maandishi yao, yanaweza kutuongoza kwake pekee ambaye ana maneno ya uzima wa milele!

Mwisho

Twende kwa nani?

Jibu lazima liwe "Yesu!"

Yeye ndiye "…*Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai*".

Yeye pekee ndiye aliye na "…*maneno ya uzima wa milele*".

Utampata wapi Yesu?

Si katika maneno ya wanatheologia wa kisasa na watengeneza picha, ambao wamejaribu kumtengeneza Yesu kulingana na sura zao wenyewe.

Lakini katika maneno ya mitume Wake, mashahidi wa ukuu wake na kuvuviwa na Roho ili kutufunulia yote tunayohitaji kwa ajili ya uzima na utauwa.

Usiruhusu machafuko ya sauti za kisasa zikupoteze kutoka kwa Yesu na maneno yake ya uzima wa milele. Hakikisha kwamba ni maandishi ya mitume wake, neno la Mungu, inayokuongoza kwake yeye aliye njia, kweli na uzima!